


# Uadilifu Kwa Taifa Lenye Haki



"Nia yetu ni kufanya vema, si mbele ya Bwana tu, lakini pia mbele ya watu."  
2 Wakorintho 8:21

**KAMPENI YA KWARESIMA  
2024**





© KCCB-CPIHD - Idara ya Kikatoliki ya Haki na Amani, 2024

**Ubunifu na utayarishaji:**

Makao Makuu ya Baraza la Maaskofu Wakatoliki wa Kenya

Idara ya Kikatoliki ya Haki na Amani

**Wahariri:** Eusebius Atamallo, Festus Rotich na Wainainah Kiganya

**Uchoraji:** Robert Kambo

**Usanifu na upambaji wa kurasa:** Kelvin Malombe

**Mratibu wa michango:** Constance Ikhabi Mutende

**Wapigaji chapa:** Don Bosco Printing Press, S.L.P. 158 Makuyu 01020, Kenya;  
boscoprint@donbosco.or.ke

**UADILIFU KWA  
TAIFA LENYE HAKI**  
KAMPENI YA KWARESIMA YA 2024

# YALIYOMO

- 5 **DIBAJI: UADILIFU KWA TAIFA LENYE HAKI**  
8 **UTANGULIZI: KWARESIMA KATIKA KANISA KATOLIKI**  
9 **UFAFANUZI: VITUO VYA NJIA YA MSALABA**
- 13 **WIKI 1: MAMLAKA YA WANANCHI**  
13 TAZAMA: SIMULIZI  
13 AMUA: UTATHMINI WA HALI HALISI  
14 TAFAKARI YA KIROHO  
15 TENDA: MASWALI YA KUWAZIA  
15 KUJICHUNGUZA  
15 MATENDO YALIYOPENDEKEZWA
- 17 **WIKI 2: HAKI YA MAJI SAFI NA YA KUTOSHA**  
17 TAZAMA: SIMULIZI  
17 AMUA: UTATHMINI WA HALI HALISI  
19 TAFAKARI YA KIROHO  
20 TENDA: MASWALI YA KUWAZIA  
20 KUJICHUNGUZA  
20 MATENDO YALIYOPENDEKEZWA
- 22 **WIKI 3: CHANGAMOTO ZA GHARAMA YA JUU YA MAISHA**  
22 TAZAMA: SIMULIZI  
22 AMUA: UTATHMINI WA HALI HALISI  
23 TAFAKARI YA KIROHO  
25 TENDA: MASWALI YA KUWAZIA  
25 KUJICHUNGUZA  
25 MATENDO YALIYOPENDEKEZWA
- 27 **WIKI 4: IMANI KALI ZA KIDINI**  
27 TAZAMA: SIMULIZI  
28 AMUA: UTATHMINI WA HALI HALISI  
29 TAFAKARI YA KIROHO  
30 TENDA: MASWALI YA KUWAZIA  
30 KUJICHUNGUZA  
30 MATENDO YALIYOPENDEKEZWA
- 32 **WIKI 5: VITISHO IBUKA KWA FAMILIA**  
32 TAZAMA: SIMULIZI  
32 AMUA: UTATHMINI WA HALI HALISI  
33 TAFAKARI YA KIROHO  
35 TENDA: MASWALI YA KUWAZIA  
35 KUJICHUNGUZA  
35 MATENDO YALIYOPENDEKEZWA
- 77 **SALA KWA KADINALI OTUNGA**  
78 **SALA YA KAMPENI YA KUPIGANA NA UFISADI**

### UADILIFU KWA TAIFA LENYE HAKI

**K**waresima ni msimu wa kutafakari, kusali, kufunga, kutubu na kuwa wafadhili. Mungu wetu mwenye huruma huwa nasi kila mara akituonyesha upendo wa milele kupitia kwa upatanisho wa binafsi na wengine na vyote alivyoviumba. Tukiwa Kanisa Katoliki, huu ni msimu maalumu unaotukumbusha kwamba maisha yetu duniani si ya kudumu.

Msimu huu wa Kwaresima umewadia wakati wa kihistoria kwani Kanisa Katoliki limeakisi kujiimarisha na kuleta kila mtu pamoja na kila mmoja kumsikiliza mwingine. Moyo wa kusikiliza sauti ya kila mtu aliye sehemu ya Kanisa unatuwezesha kushikana kama jamii moja, inayoshiriki kikamilifu katika maisha na utume wetu unaotualika kuwa mashahidi wa Kristo aliyefufuka. Safari ya kumshirikisha kila mtu inatupatia fursa nzuri ya kuwa mashahidi wa Mungu hadi mwisho wa dunia (Matendo 1:8). Ndiposa tunaalikwa kuendelea kuuomba utaratibu huu wa kutilia mkazo kutambulika kama Kanisa ambalo linashirikisha wote, iwe ni fursa ya mashauriano ya kulifanya Kanisa kumpatia Kristo kipaumbele katika kila tunalolifanya na kutambulikana kama wana wa Mungu.

Tafakari za Kwaresima mwaka huu zinaangazia kiini cha imani ya Kikristo: kuwajali na kuwatunza maskini. Katika mafundisho yake, ada na sala, maskini wamo katika kiini cha utumishi wa Kanisa. Maudhui ya mwaka huu, **Uadilifu kwa Taifa lenye Haki**, inaakisi utumiaji wa uadilifu kuweka misingi thabiti ya haki Kenya. Taifa lenye haki hujengwa na watu waadilifu. Ndiposa tunaalikwa kutafakari juu ya safari yetu ya imani tukiwa watu wa Mungu waliobatizwa na wanaoishi kwa uadilifu ili kujenga taifa lenye haki.

Msimu huu wa Kwaresima unatupatia jukumu la kufanya mambo yetu yote kwa uadilifu. Tukiwa watu wanaojali maadili, hatuna budi kupigania haki za maskini. Kuna mengi muhimu ambayo tukiwa Wakristo tunaombwa kutetea. Hata hivyo, Mama Kanisa anasema tuna hiari moja tu kwa maskini; kuwapatia kipa umbele. Maskini ni nani? Wajane na mayatima wametajwa katika Agano la Kale kuwa watu walio katika mazingira magumu katika jamii. Yesu katika mafundisho yake mlimani anatangaza: "Heri walio maskini wa roho, maana Ufalme wa Mbinguni ni wao." Anaonyesha madhara ya kuwapuuzwa maskini katika simulizi lake kuhusu mfano wa tajiri na maskini aliyelitwa Lazaro. Vitabu vingi vya kinabii vinalaani

ukandamizaji wa maskini na kuhimiza watendewe haki. Kwenye mfano wa Msamaria Mwema, Yesu anasisitiza tuwapende na kuwatumiza majirani zetu, hasa walio na shida.

### **Maandiko matakatifu yanasema nini kuhusu uadilifu?**

Zaburi 25:21 ni sala ya ulinzi mtakatifu kwa misingi ya mema ya uadilifu na uaminifu. Uadilifu ni nguzo kuu ya mafundisho ya Kanisa, na ishara ya kuwajali wengine kwa dhati. Isaya 1:17 inatuhimiza tujifunze kutenda mema, tutafute haki, tuwatie moyo walioonewa na kuwatetea mayatima na wajane. Mika 6:8 inasisitiza kuwa uadilifu unapaswa kuambatana na kutenda kwa haki, kupenda rehema, na kwenda kwa unyenyekevu na Mungu na wanadamu.

Baba Mtakatifu Francis, akiongoza kwa mfano katika unyenyekevu na usahili wake, anasisitiza umuhimu wa kutumia maskini na waliotengwa kwa matendo yanayozingatia kanuni za haki na uadilifu. Mama Teresa alikuwa kielelezo cha unyenyekevu kwa kujitolea kutumikia maskini na kuishi kwa uadilifu na haki.

Vipimo saba muhimu vya uadilifu katika maisha ya kila siku ni uaminifu na imani; uwazi; kuzingatia kanuni za maadili; uwajibikaji; unyenyekevu; ujasiri; na maamuzi ya kimaadili na kujitolea kutenda yaliyo sahihi.

Kama ilivyoenezwa wazi katika mafundisho ya Kikatoliki kuhusu jamii, kuwapatia maskini kipa umbele kuna maana kwamba hatuwezi kuwaacha waonewe na kutafuta vijisababu vya kutochukua hatua kuwasaidia. Umaskini wetu wa kiroho unapasa kuamsha dhamiri zetu kuchukua hatua za kuwaondolea maskini mateso na dhiki ya umaskini. Tunaalikwa kuwa maajenti wa kuhakikisha tuna taifa lenye haki.

Haki ya jamii inasisitiza ugavi wa haki wa rasilimali, nafasi na manufaa kwa jamii. Yanatuhimiza sote kukataa mambo ambayo hayaleti usawa wala kuimarisha manufaa kwa wote. Katika **Wiki ya Kwanza**, tunaangazia **mamlaka ya wananchi** kama yanavyolindwa na Katiba. Huduma bora za umma ni haki ya Wakenya wote.

Suala la **haki kwa jamii** limetiliwa mkazo katika **Wiki ya Tano**. Wanadamu wakikosa hali nzuri ya maisha, familia nyingi hazitaweza kukabiliana na vitisho vingi vinavyokumba dhana ya familia kama ilivyoteuliwa na Mungu. Maendeleo ya kiteknolojia pamoja na kile Baba Mtakatifu Francis anakiita “udikteta wa imani kuwa maarifa na maadili ni mambo ya mpito yanayotawaliwa na fikira zetu na wakati” ni vitisho halisi kwa familia.

**Wiki ya Pili** inaangazia **Haki ya maji safi na ya kutosha**. Ufahamu kamili wa mazingira, kanuni za haki na uhusiano kati yetu na mazingira hutuwezesha kuuelewa wajibu wetu kulinda mazingira.

Ugavi sawa wa rasilimali, manufaa na mizigo ya jamii ni haki ya Wakenya wote. Baraza Kuu la Maaskofu Wakatoliki Kenya limeangazia suala hili katika nyaraka zake za kitume za awali na taarifa kwa wanahabari. **Wiki ya tatu** inaangazia **gharama ya juu ya maisha** na kodi za juu. serikali inahitaji kuwajibika na kuzingatia uwazi katika matumizi ya kodi inazotoza wananchi.

Haki ya kuabudu ni suala muhimu. Lakini kama tunavyoakisi katika **Wiki ya Nne**, matendo ya kutisha ya madhehebu yanatumia dini kutenda ukatili wa imani kali za kidini, kama ilivyoshuhudiwa katika Shakahola na sehemu nyingine, hayawezi kukubalika.

Kanisa katika harakati za sasa kutilia mkazo kutambulika kama Kanisa linaloshirikisha kila mtu, Wakristo wanaalikwa kuunga na kuyapatia kipa umbele mahitaji ya maskini. Tunahimizwa kuimarisha ushirika kati yetu na kuhusika kikamilifu katika maisha ya Kanisa kuanzia kwa familia kukubali wito wa kuwa mashahidi wa Kristo. Tutafute wasaa wa kutafakari, kubadili nyendo, kutenda ufadhili na kutimiza wajibu wa kuwasaidia maskini kwa kubomoa miundo ya jamii ambayo haiendelezi usawa.

Neema za msimu huu wa Kwaresima zitufanye kuwa vyombo bora zaidi vya wito wa Mungu kuwa mashahidi wa haki ya jamii miongoni mwa majirani zetu, katika kaunti na nchini. Kufika mwisho wa siku 40 za sala, kutubu na kumrudia Mungu, tuuangazie muujiza wa Pasaka kwa ukarimu na kufufuka pamoja na Kristo aliyefufuka.

**Rt Rev John Oballa Owa**

*Mwenyekiti, KCCB-CPIHD*

*Idara ya Kikatoloki ya Haki na Amani*

*Askofu wa Ngong*

## UTANGULIZI

### KWARESIMA KATIKA KANISA KATOLIKI

**K**waresima ni kipindi cha siku 40 cha kufunga na kujinyima, kusali na kutubu kabla ya Pasaka. Kulingana na utamaduni wa Kikristo, msimu huu katika mwaka wa kiliturjia huanza Jumatano ya Majivu na kumalizika Jumapili ya Matawi. Ni adhimisho la kila mwaka ambalo huwatayarisha waumini – kupitia sala, toba, kutoa zaka na kujinyima – kwa matukio yanayohusiana na mateso ya Yesu msalabani, na maadhimisho ya ufufuko wake. Wakatukumeni hubatizwa Jumapili ya Pasaka.

#### **Kwa nini siku 40?**

Nambari 40 ni muhimu katika maisha ya Wakristo. Musa na wana wa Israeli, kwa mfano, walitanga jangwani kwa miaka 40 wakijiandaa kwenda katika nchi waliyoahidiwa na Mungu. Musa alikaa juu ya Mlima Sinai kwa siku 40 bila kula wala kunywa alipokuwa ameenda kupokea vibao vya mkataba ambao Mungu aliwawekea Waisraeli. Nyakati za Nuhu, gharika iliendelea kwa siku 40 mchana na usiku. Eliya alikaa siku 40 mchana na usiku juu ya Mlima Horebu bila chakula. Yesu naye alienda jangwani na kufunga kula na kunywa kwa siku 40 mchana na usiku.

#### **Asili ya Kampeni ya Kwaresima Kenya**

Kuzingatia wito wa kiroho wa msimu wa Kwaresima, Kanisa Katoliki katika Kenya liliazimia kuwapasha waumini habari kuhusu matatizo yanayokumba jamii na kushirikiana nao kutetea mabadiliko. Kupitia kwa Kampeni ya Kwaresima, Maaskofu wa Kanisa Katoliki huwaita Wakristo wote na watu wa mapenzi mema kuungana na kukabiliana na matatizo hayo, huku wakitetea mabadiliko. Kwa kuungana na maaskofu katika utetezi huo wa mageuzi, juhudi za kila mtu binafsi pamoja na sauti ndogo ya kila mmoja ikiunganishwa na ya wengine husikika mbali, nayo matendo ya kila mmoja huongezeka yakijumuishwa na ya wengine.



# UFAFANUZI

## VITUO VYA NJIA YA MSALABA

### **KITUO CHA 1: Yesu ahukumiwa kifo**

Tunamwona Yesu akiwa amevishwa taji la miiba kichwani akitokwa na damu, huku mikono yake imefungwa kutoka nyuma. Nguo zake zimeshikana na vidonda vyake. Pilato anachukua maji na kunawa mikono yake mbele ya umati wa watu akisema: "Sina hatia juu ya damu ya mtu huyu, hili ni jukumu lenu!" Sisi pia hufanya vivyo hivyo. Tunawafunga wengine kwa maoni yetu na kuwadhalilisha kwa kutumia vibaya mamlaka yafaayo kuwainua wala si kuwaingiza utumwani. Tunaomba kuwa walio mamlakani wasitufunge mikono na kutuzuia kuinua maisha yetu.

### **KITUO CHA 2: Yesu aubeba msalaba wake**

Tunatafakari kuhusu uzito wa msalaba na jinsi unavyo yaumiza mabega yake baada ya kupewa hukumu ambayo haikustahili. Ni mara ngapi huwa tunawabebesha mizigo mizito marafiki zetu na wengine walio karibu nasi kwa matendo yanayosababisha usumbufu kama vile uchafuzi, utumiaji mbaya wa mali asili, kutupa ovyo takataka na kuharibu vianzo vya maji safi na salama ya kunywa? Tuombe tuwe wasimamizi bora wa mali tulizopewa na Mungu kutunza kwa manufaa ya wote.

### **KITUO CHA 3: Yesu anaanguka kwa mara ya kwanza**

Tunaushuhudia unyonge unaojionyesha katika macho yake, mwili wake uliochoka hadi akaanguka chini, huku akihangaishwa na askari wakijaribu kumwinua. Sisi pia hujipata katika hali sawa maishani. Kuna masuala yanayotubwaga chini kama vile changamoto za gharama ya juu ya maisha zinazotuzidishia magunu maishani. Yesu anatupatia nguvu za kuichunguza hali yetu kwa matumaini. Tuombe kuwa walio na uwezo wawasaidie maskini na walio mamlakani washughulikie gharama ya juu ya maisha inayowalemea maskini.

### **KITUO CHA 4: Yesu akutana na mamake**

Tukiwatazama, tunatafakari kuhusu muujiza wa uwezo wa upendo kumpatia mtu nguvu za kushinda masaibu ya maisha, vurugu, chuki, utengano na kukata tamaa. Ni mara ngapi huwa tunawaonyesha upendo watu wakiwa katika hali mbaya, wanapokataliwa, kueleweka vibaya, na hata kusingiziwa maovu bila hatia au kutoka kwa familia ambazo baadhi ya watu wake wana imani kali za dini zinazowaathiri wengine? Tuombe tusaidiwe kuepuka ubaguzi kwa misingi ya dini; kwamba kwa vile sote tumeumbwa kwa mfano wa Mungu, tunapaswa kujiepusha na maovu kama vile ulanguzi wa binadamu, kung'oa watu viungo vya mwili na imani kali za dini. Tuombe tupate uwezo wa kuwaona wengine wote kuwa viumbe wa Mungu, tupendane, tutambue na kulinda utukufu wa maisha.

### **KITUO CHA 5: Simon wa Cyrene amsaidia Yesu kuubeba msalaba**

Tunautazama uso wake uliojaa huzuni kana kwamba anaomba msaada wetu, huku tukitafakari kuhusu mateso anayopitia. Ni muhimu kutambua jinsi anavyomtazama Simon kwa unyenyekevu na shukrani. Yesu anatumkumbusha kuwa kuna nyakati tunahitaji misaada ya wengine bila kushuku nia zao. Tunahimizwa kuingia katika maisha ya wanaopitia magumu wakijaribu kukimu maisha, wale ambao familia zao zimo katika hatari ya kusambaratika na walionyimwa hadhi ya binadamu. Tunaalikwa kudumisha mshikamano na kutambua nguvu za umoja kwa manufaa ya familia zote, wenye tatizo la utumiaji mbaya wa dawa za kulevya, au wanaoshiriki umalaya na maovu mengine yanayokumba familia.

### **KITUO CHA 6: Veronica ampangusa Yesu usoni**

Tunaona nini tunapoutazama uso wa Yesu? Unatuonyesha nini? Tunaona nini tunapotazama kwa undani dhiki na machungu ya wengine? Tunaweza kuwakubali walio taabani? Waliofunikwa uso kwa dhiki na machungu?

### **KITUO CHA 7: Yesu anaanguka kwa mara ya pili**

Tunamtazama Yesu akiwa chini na kutafakari machungu anayoyapitia. Tunamwonea huruma na kufahamu kwamba hatutawahi kamwe kujiona tukiwa pekee yetu tukikabiliwa na mateso. Tumwombe atusamehe kwa kukosa kumtegemea. Ee Mungu, tupe nguvu za kutuwezesha kukabiliana na wasiwasi, huzuni, machovu, matatizo ya akili na magonjwa. Tuendeleo kukutegemea kama asili ya matumaini ili tuzidi kukutumikia ipasavyo.

### **KITUO CHA 8: Yesu akutana na wanawake wa Yerusalemu**

Tunapotazama nyuso zao, tunaona zilivyojaa upendo na shukrani, majonzi na woga. Tunashangazwa na yaliyofanyika kati yao. Upendo wake uliojaa huruma kwetu unatuweka walipo wanawake na watoto waliomwonyesha upendo na huruma. Bwana, wanawake wa Yerusalemu wanatumkumbusha kwamba hata wanaoteseka wana hadhi na ni wanao. Tunaomba utuwezeshe kurejesha thamani ya utu bila kuhusudu mali, teknolojia, serikali, rangi ya ngozi, asili na matendo mengine yanayoharibu sura ya ulimwengu.

### **KITUO CHA 9: Yesu aanguka kwa mara ya tatu**

Tunatafakari kuhusu hali yake akiwa chini; mateso yanayotufanya sisi kukamilika, jinsi alivyokubali hali yake ili kutupatia uhai. Tunatafakari ili kupatana na kuupokea upendo wake kamili. Amejitolea kabisa kwetu. Bwana, tuwezeshe kufuata maagizo yako ya huruma, ukarimu na upendo. Mara nyingi huwa tunapuuza maagizo hayo. Tunakuomba utuonyeshe njia yako ili ibaki kuwa chanzo cha nguvu zetu katika matatizo na mateso.

### **KITUO CHA 10: Yesu anapokonywa mavazi yake**

Tunashuhudia akivuliwa mavazi na kukabiliana na mauti akiwa uchi. Tunatafakari anavyojifichua kwetu, bila kuficha chochote. Bwana, umetualika tuje kwako bila kuficha chochote ili kurejelea hali ya awali ya mwanadamu ambapo hakuwa na hatia. Tumevaa maringo, kutotii,

unyanyasaji na maovu ambayo yamefanya maisha ya wengine kuwa magumu. Tujengee jamii inayokupendeza na kuwahudumia wengine, kuendeleza umoja na kukuabudu.

### **KITUO CHA 11: Yesu asulubiwa msalabani**

Tunashuhudia akipigiliwa misumari msalabani. Je, tukiutazama uso wake tunaona kama kuna uchungu na dhiki ambayo hawezi kufahamu? Bwana, hata nasi huwasulubisha ndugu zetu, tunakataa kuwasamehe, kuwasaidia au kushirikiana nao kujenga jamii ya upendo. Nyoyo zetu zimejaa chuki na roho wa kisasi. Tusaidie kuachana na yote hayo kwa kusameheana kwani tunaposamehe nasi husamehewa.

### **KITUO CHA 12: Yesu anakufa msalabani**

Tunasimama pale chini ya msalaba na kuukumbatia ukombozi wetu. Hapo, tunashuhudia anayetupatia uhai akiingia katika mauti. Bwana, huwa tunakumbana na vifo vidogo katika chuki, familia zilizovunjika, vurugu na kutoelewana. Ndani ya kila mmoja wetu kuna jeraha la kutofaulu, kuaibishwa na nia mbaya. Kupitia kwa kifo chako, tunaomba utubadilishe ili tuwe chanzo na nguvu za ubunifu ambapo ushirika, urafiki na uelewano zitapata kipa umbele.

### **KITUO CHA 13: Yesu atolewa msalabani**

Tunashuhudia akitolewa msalabani na kutamani kuugusa na kuupapasa mwili wake. Tunakumbuka yote ambayo mikonu yake iligusa, wote aliowakumbatia na kuwaletea baraka, tunatafakari na kuacha yote hayo yazame ndani mwetu. Anafahamu muujiza wa mauti. Ameingia katika mikono mizuri. Bwana, tunakumbuka maneno ya mtumishi wako Ayubu. Ninajua kwamba Mkombozi wangu yu hai. Nami baada ya ngozi yangu kuharibiwa, bado nikiwa na mwili huu nitamwona Mungu; mimi nitamwona kwa macho yangu mwenyewe ... (Ayubu 19:25-27). Tusamehe kwa kuwa mara nyingi tunaishi tukijifikiria tu sisi wenyewe; katika maisha yetu, tunajijali tu sisi wenyewe, kazi zetu, tamaa zetu na mambo tunayoyaogopa. Tunaomba upande ndani yetu moyo mkubwa wa kujali na uliojaa ukarimu. Tusaidie kuwajali wote walio karibu nasi.

### **KITUO CHA 14: Yesu alazwa kaburini**

Tunasimama kwa muda nje ya kaburi lake. Safari hii yake ya mwisho duniani imetuonyesha maana ya zawadi yake mwenyewe kwetu. Kaburi lake linawakilisha kila kaburi tunalokabili kwa woga na kung'ang'ana kuamini huenda kaburi halina maiti. Bwana, ulitufundisha kwamba maisha ya milele ni kumjua Mungu na Yesu ambaye alimtuma kwetu. Tupe moyo wa kujitolea, imani na upendo; kujitolea kwa maisha ya wanadamu wote na hasa walio dhaifu na wanyonge. Tusaidie kuonyesha wengine maana ya uhai wa milele, upendo na imani inayotusaidia kushinda woga wa mauti.

*Kiongozi: Tunakuhusudu Kristo na kukubariki.*

*Wote: Kwa sababu kwa msalaba wako umeukomboha ulimwengu*



**SIKU YA WAKAZI WA ENDELEU**

**AGENDA**

- Uandilizi wa Bajeti
- Ripoti ya ukaguzi wa hesabu



Njaa




Hali mbaya ya kiuchumi

**UKUMBI WA JAMII WA ENDELEU**



**KAMATI YA UANGALIZI WA MASUALA YA UMMA**



## WIKI 1

# MAMLAKA YA WANANCHI

### **TAZAMA: SIMULIZI**

**M**ji wa Endelevu ulijivunia ustawi wa kiuchumi chini ya uongozi ulioheshimu umuhimu wa mamlaka ya wananchi. Mashirika yote ya serikali yalishirikiana na raia katika shughuli zake na kuwashirikisha kikamilifu katika kuinua kiwango cha utoaji huduma.

Lakini baada ya muda, uchumi wa Endelevu ulianza kuzorota baada ya uongozi uliopuuza mamlaka ya wananchi kuchukua mamlaka. Viongozi wavya hawakujali uongozi wa sheria, wakapuuza mpango wa kuwashirikisha raia katika uandalizi wa miradi ya umma na shughuli za serikali. Raia walikata tamaa na kupuuzilia mbali ushirika wao katika shughuli za uandalizi wa bajeti kwa kuamini hakuna mabadiliko yoyote yangefanyika.

Ili kubadilisha mambo na kuuondoa uongozi mbaya, viongozi wa dini na wengine katika jamii, wakishirikiana na vijana na wazee mjini, waliandaa vikao vya kuhamasisha na kuelimisha raia kuhusu umuhimu wa kurejesha na kuimarisha uwajibikaji, uongozi unaoleta mabadiliko hitajika na kuwashirikisha ipasavyo katika shughuli zake. Matokeo ya juhudi hizo yakawa kuinuka kwa kiwango cha ufahamu wa raia kuhusu mamlaka yao, wakabuni kamati za kusimamia miradi ya umma, na hasa mkakati wa kufufua uchumi wa Endelevu. Walifanya ukaguzi wa kijamii wa taratibu za serikali za ununuzi wa bidhaa na huduma, wakahakikisha ubora wake na kuwa pesa za serikali zinatumiwa kwa miradi ya kuwanufaisha wote. Walibuni kamati za usimamizi wa miradi ya umma na wakaimarisha elimu ya kila mara kwa raia ili kuinua ushirika wao katika masuala ya umma. Raia walifahamu zaidi kuhusu haki zao na majukumu, wakapata nguvu mpya za kushiriki katika masuala ya umma, kiwango cha huduma za umma, uwajibikaji na uwazi kikaimarika na hali ya maisha ikainuka.

### **AMUA: UTATHMINI WA HALI HALISI**

Kenya ilipopata uhuru 1963, iliaminika ilikuwa na Katiba bora iliyotenganisha ipasavyo mamlaka ya idara tatu kuu za serikali na kulinda mfumo wa serikali za majimbo. Kati ya 1964 na 1991, Katiba

hiyo ilifanyiwa angalau mabadiliko 26, mengi yake yakilenga kumpatia Rais uwezo zaidi, kudhoofisha Mahakama na Bunge, kuzipokonya mamlaka asasi zote za kuimarisha demokrasia, haki za binadamu na uhuru. Hata hivyo, Wakenya waliamka, wakapigana na uongozi dhalimu na kidikteta mpaka wakapata mfumo mpya.

Mamlaka yote makuu Kenya ni ya wananchi na wanayatekeleza moja kwa moja au kupitia kwa wawakilishi wao waliochaguliwa kidemokrasia kuzingatia Sura ya Kwanza ya Katiba ya 2010. Hata hivyo, kati ya 2013 na 2022, wanasiasa wameendelea kuwapokonya wananchi haki zilizohifadhiwa na Katiba. Serikali ya kitaifa imeendelea kuchelewesha pesa zilizotengewa kaunti na hivyo kukwamisha maendeleo. Visa vya wizi na utumiaji mbaya wa pesa nyingi za umma vimeendelea kuripotwa, malalamiko ya utoaji wa kazi za serikali kikabila yamezidi, Serikali ya kitaifa kudhoofisha asasi huru, kuwahonga wapigaji kura na kuongeza kodi za serikali.

Uongozi wa Kenya unahimizwa kulinda mamlaka ya wananchi. Rasilmali za kitaifa husimamiwa kwa manufaa ya wananchi wote. Sheria ya Haki inalinda na kuimarisha haki zetu za kisiasa, kiraia, kiuchumi, kijamii na kitamaduni. Utekelezwaji wa haki hizi ni thibitisho la ahadi ya demokrasia yetu na hakikisho la ugavi wa haki wa rasilmali za kitaifa. Wakenya wana mamlaka ya kuwafuta kazi wabunge na wawakilishi wa wodi, na kumfungulia Rais mashtaka. Tukae macho kuhakikisha mamlaka ya wananchi yanaheshimiwa.

Kulingana na *Mafundisho ya Kanisa Katoliki Kuhusu Jamii*, watu wote wana haki ya kushiriki katika masuala ya kiuchumi, kisiasa na kitamaduni ya jamii. Kwenye hotuba yao kuhusu hali ya taifa waliyoitoa Mei 27, 2022, Maaskofu Wakatoliki Kenya walisisitiza umuhimu wa kuinua uwezo wa raia kutumia upigaji kura kama fursa ya kuchagua viongozi wenye busara ili kuhudumia na kuwaongoza Wakenya kuishi pamoja kwa amani. Walishauri kuwa afisi za umma hazifai kuwa nafasi ya wanaozishika kujitajirisha kibinafsi na kuvunja kiholela haki za raia.

## **TAFAKARI YA KIROHO**

**Mwanzo 9:8-15**

**1 Petero 3:18-22**

**Mariko 1:12-15**

Mungu aliweka agano na wanadamu na viumbe vyote hai kwamba kamwe hatawaangamizwa kwa gharika.

Kila kitu kinapaswa kuwa kwa manufaa ya viumbe wa Mungu na sio kwa maangamizi. Hayo ni pamoja na mamlaka ya kisiasa yanayofaa kutumiwa kwa manufaa ya wote. Ni juu ya wanadamu kuwachagua viongozi wao kwa kuzingatia ada za maadili na sheria takatifu. Baada ya kuokolewa kutokana na maovu ya dunia kwa maji ya ubatizo, tunaweka agano jipya la kuishi tukizingatia mapenzi ya Mungu kwa kutambua mamlaka yake, huku tukitekeleza haki zetu na majukumu tukizingatia uwajibikaji na ufahamu mpya.

Katika Injili, baada ya kuzima juhudi za shetani kuhujumu kazi ya Mungu, Yesu anatangaza kuwa wakati umewadia wa kutimiza ahadi za Mungu. Siku 40 jangwani zinawakilisha msimu wa majaribio. Jamii yetu inajaribiwa. Katika maamuzi na matendo yetu ya kila siku, tufahamu kuwa ndani ya Kristo tutashinda hatimaye.

Yesu anawasilihi watu kutubu na kuziamini habari njema. Anatuonyesha Ufalme wa Mungu ambao sote tunauhitaji ili kuhakikisha mamlaka ya wananchi yananufaisha kila mtu na wote katika jamii msimu huu wa Kwaresima.

### **TENDA: MASWALI YA KUWAZIA**


- » Je, ufahamu vile mamlaka ya raia yanalindwa na Katiba?
- » Je, Kanisa na wadau wengine wana jukumu gani katika kutetea ushirikishwaji kamili wa raia?
- » Je, nina wajibu gani katika kutetea haki na maslahi ya waliotengwa na walio kwenye mazingira magumu Kenya?

### **KUJICHUNGUZA**

- » Nimekuwa nikiyatumiaje mamlaka yangu? Je, nimeheshimu au kudhoofisha mamlaka ya wengine?
- » Je, ninaufahamu usimamizi wa mamlaka ya Wakenya?
- » Je, ninahakikishaje watumishi wa umma wanatenda na kutumia mamlaka kwa kuwajibika, kujali uwazi na maadili?

### **MATENDO YALIYOPENDEKEZWA**

- » Shiriki harakati za mashirika ya kidini kuelimisha watu kuhusu mamlaka ya wananchi.
- » Andaa matembezi Jumamosi ya wiki inayoangazia mamlaka ya wananchi na upande miti ya ukumbusho.
- » Shiriki katika shughuli zinazolenga kuiimarisha jamii.





## WIKI 2

# HAKI YA MAJI SAFI NA YA KUTOSHA

### **TAZAMA: SIMULIZI**

**K**ijiji cha Maji Matamu chini ya vilima vya Divani vyenye rasilmali nyingi hakikuwahi kukosa maji safi na yaliyotosha wote ya chemichemi. Chanzo hicho cha maji kiliwawezesha wanakijiji kulima katika majira yote. Eneo lote lilizingirwa na msitu uliojaa mimea na miti iliyosifika kwa dawa zake nadra za kiasili na ambazo wanakijiji walitumia kubadilishana na bidhaa nyingine kutoka maeneo ya mbali.

Kampuni mbili ziliruhusiwa kujenga vilimani ili kuchota na kupakia maji safi kutoka kwa chemichemi, na kutengeneza dawa kutoka kwa mimea msituni. Wazee waliotoa kibali hicho waliamini shughuli za kampuni hizo mbili zingenufaisha wanakijiji.

Mambo yalikuwa mazuri siku za mwanzo na wanakijiji walijiinua kimaisha kwa mapato kutoka kwa kampuni hizo. Lakini mwaka mmoja baadaye, waligundua chemichemi waliyoitegemea ilishaanza kukauka na maji yake kuchafuliwa. Mimea yao ikaanza kunyauka hata ikinyunyuziwa maji. Kampuni ya dawa ilikuwa imekata miti karibu yote na misimu ya anga ikabadilika.

Wanakijiji waliolalamika walizimwa kikatili na wazee wa kijiji walionufaika zaidi na shughuli za kampuni hizo. Viongozi wa kidini waliungana na wanakijiji kupigania mabadiliko na kulinda chanzo chao cha maji na riziki. Hatimaye, wanakijiji walifanikiwa kuchagua wazee wengine. Jamii ikiongozwa na viongozi wa kidini na wengine wenye ushawishi mkubwa, ilikutana na wawakilishi wa kampuni na kukubaliana kuhusu ugavi wa maji kwa manufaa ya wote. Shughuli haribifu za kampuni ya dawa zilisimamishwa. Wanakijiji walipanda miti katika maeneo yaliyoachwa wazi na wakazindua pia miradi ya kulinda msitu na chemichemi.

### **AMUA: UTATHMINI WA HALI HALISI**

Baadhi ya sehemu za Kenya hupata mvua nyingi mara kwa mara kila mwaka. Wanadamu na viumbe wengine hupoteza maisha, huku mimea na mali zikiharibiwa na mafuriko. Kiasi kikubwa cha maji hayo safi ya mvua huishia kwenye maziwa na bahari kwani hatuna mbinu za kuyatega na kuyahifadhi kwa matumizi ya siku zijazo. Misimu ya mvua nyingi mara nyingi hufuatiwa na vipindi

virefu vya kiangazi. Mimea hukauka na wanyama kufa kwa kukosa chakula na maji. Madhara yanayosababishwa na mafuriko na kiangazi ni ishara bayana ya udhaifu wa mikakati yetu ya kukabiliana na majanga.

Kenya ina vianzo 88 muhimu vya maji vilivyotambuliwa na Kenya Water Towers Agency. Hata hivyo, ni vianzo 18 pekee vinavyolindwa na sheria, ikiwa ni pamoja na Mau Complex, Mlima Kenya, Aberdare Ranges, Cherangany Hills na Mlima Elgon. Vianzo hivyo ni asili muhimu ya mito 13 mikubwa kama vile Ewaso-Ng'iro, Mara, Makalia, Amalo, Molo, Mumberes, Naishi, Nderit, Njoro, Nzoia, Nyando, Sondu na Yala. Maji kutoka kwa mito hiyo huishia katika maziwa matano muhimu Kenya na nchi jirani. Ziwa Victoria ni mojawapo ya maziwa hayo na ni chanzo cha Mto Nile ambao huishia katika Bahari ya Mediterranean. Mto Nile ni tegemeo la maisha kwa mamilioni ya watu katika Uganda, Sudan Kusini, Sudan na Misri.

Yasikitisha kukuta kwamba karibu Wakenya milioni 28 hawana maji safi, huku wengine milioni 41 wanakabiliwa na athari za mazingira chafu. Kenya inakabiliwa na changamoto kubwa ya uhaba wa maji, huku mahitaji ya bidhaa hiyo muhimu yakizidi kuongezeka. Mabadiliko ya hali ya anga, ongezeko la watu, ustawi wa miji, uchafuzi wa maji na usimamizi mbaya wa vyanzo vya maji zimechangia kuzorotesha tatizo la uhaba wa maji safi na ya kutosha nchini. Hali hiyo imeathiri shughuli za kiuchumi, uwezo wa nchi kujitosheleza kwa chakula, elimu na afya.

Suala la maji safi na usafi wa mazingira ni la sita kwenye orodha ya Malengo 17 ya Ustawi Endelevu (SDGs) ya Umoja wa Mataifa. Siku ya Maji Duniani huadhmishwa kila Machi 22. Haki ya maji safi, salama na ya kutosha imehifadhiwa katika Kifungu 43 (d) cha Katiba. Shirika la Water Services Regulatory Board (WASREB) husimamia umiliki, utumiaji na usimamizi wa rasilmali na huduma za maji. Ingawa utoaji wa maji safi, salama na ya kutosha ni jukumu la serikali zote 47 za kaunti, hakuna kaunti yoyote imefikia lengo hilo.

Baba Mtakatifu Francis ameliangazia suala la maji katika waraka wake wa kitume, *Laudato Si*. Anasema: "Huduma za maji (suala ambalo ni muhimu sana) zilikuwa za kutegemewa lakini sasa katika maeneo mengi, mahitaji yamezidi utoaji endelevu wa bidhaa hiyo, na hivyo basi kusababisha athari kubwa katika kipindi kifupi na muda mrefu pia" (*Laudato Si no.28*). Anaonya kuhusu tatizo kubwa

la uhaba wa maji ya kiwango cha kufaa kwa maskini. Magonjwa ya kuhara damu na kipindipindu ambayo husababishwa na mazingira chafu na uhaba wa maji safi, yanasababisha madhara mengi na vifo vya watoto wachanga. Vianzo vingi vya maji ya visima vinakabiliwa na tisho la kuchafuliwa na baadhi ya shughuli za uchimbaji madini, kilimo na viwanda, hasa katika nchi zenye sheria au usimamizi dhaifu (*Laudato Si* no. 29).

Ni lazima tujihadhari na mazoea ya utumiaji vibaya wa rasilmali ambayo humfanya mtu binafsi kuwa mbadhirifu na asijali kutumia upya rasilmali haba tulizonazo. hatufai kufikiria tu kuhusu uchafu kutoka viwandani. Sabuni na kemikali za kila aina ambazo matumizi yake ni kawaida katika maeneo mengi duniani, zimeendelea kutupwa ovyo kwenye mito, maziwa na bahari. Nyumbani, tunapoteza maji kutokana na mifereji iliyopasuka au inayoachwa bila kufungwa ipasavyo tunapooga mwili au kusugua meno. Mara nyingi huwa tunatumia maji mengi kuliko kiasi tunachohitaji. Wanaoteka maji kutoka mbali wanatambua kikamilifu thamani haswa ya kila tone.

## **TAFAKARI YA KIROHO**

**Mwanzo 22:1-2, 9a, 10-13, 15-18**

**Warumi 8:31b-34**

**Mariko 9:2-10**

Abrahamu alikuwa tayari kumtii Mungu kwa lolote lile. Anatuonyesha umuhimu wa kumwamini na kumtii Mungu katika maisha ya imani. Abrahamu anapewa jaribio kubwa zaidi maishani mwake na yuko tayari kumtii na kumwamini Mungu. Huo ndio wito tunaopewa: kumkabidhi Mungu maisha na hali yetu ya baadaye bila masharti. Majaribio hutujia maishani ili kuthibitisha mwelekeo wetu kamili katika imani na utiifu. Tunapata pia katika somo hilo Mungu wetu mwenye huruma ni Mungu wa uhai. Alimtuma malaika wake kumzuia Abrahamu kumuua mwanawe na badala yake anamwonyesha kondoo wa kutolewa kafara na hivyo basi kuokoa maisha ya Isaka. Mungu hulinda na kuendeleza maisha. Kristo, aliyetanguliwa na Isaka kubeba kuni za kumtolea kafara, alibeba msalaba ambao ungetumiwa kumtoa kafara thabiti ya kuwapatia wanadamu uhai wa milele. Tunaalikwa kutafakari iwapo tuko tayari kujitoa kwa Mungu. Mungu hutupatia upendo na msaada wake bila masharti. Yu nasi na hakuna chochote

kinachoweza kutudhuru. Upendo wa upendo wa Mungu kwetu ni jinsi alivyomtoa mwanawe kwa hiari kwa wokovu wetu.

Kupaa kwa Yesu mbinguni kunatukumbusha kuhusu utakatifu wake na mamlaka. Yeye ni chanzo cha uhai wote na mamlaka yake yanatutaka kuijali dunia yetu na viumbe vyake vyote, kwani alitupatia uhai wa milele kwa kuyashinda mauti. Na tuitii sauti yake, tukimwamini Mungu kwa ukarimu, upendo na utunzaji wake usio na masharti kwa kuyatunza maji, zawadi ya Mungu kwa manufaa ya wote. Tuyajali maumbile tuliyopewa jukumu la kuyatunza, na hasa maji na viumbe vyote ambavyo uhai wake hutegemea bidhaa hiyo.

### **TENDA: MASWALI YA KUWAZIA**

- » Ni maswala gani ya mizozo ya maji umekumbana nayo?
- » Je, maji hupatikana kwa urahisi katika eneo lako?
- » Unajua chanzo chochote muhimu cha maji katika eneo lako?

### **KUJICHUNGUZA**

- » Je, huwa ninafunga mfereji wa maji nikisugua meno?
- » Je, nimemwezesha jirani yangu kupata maji safi, salama na ya kutosha?
- » Je, huwa ninayatupa maji taka ya nyumbani ipasavyo?

### **MATENDO YALIYOPENDEKEZWA**

- » Waombe maafisa wa misitu walio karibu nawe ushauri kuhusu miti ambayo haidhuru vyanzo vya maji chini ya ardhi unayofaa kupanda.
- » Panda miti inayosaidia katika uhifadhi wa maji.
- » Tembelea afisi ya maji iliyo karibu nawe kwa maelezo muhimu kuhusu huduma za maji na uwapashe habari kuhusu urahisi au ugumu wa kupata maji karibu nawe.
- » Fanya mpango wa kushiriki kikamilifu katika sherehe za kila mwaka za Siku ya Maji Duniani.




**BEI MIPYA ZA BIDHAA**  
 HATAUZI KWIA WAKOFO KES

2KG UNGA	→	600
1KG MCHELE	→	400
1KG SUKARI	→	400

**HONGO**

**MONGI YA MAFAKI YA KALI**  
 MIPYA YA KALI  
 PAMBAZI

**KITUO CHA ICT**



**MAZIMO YA JAMII YA MZIMA**  
 0% UFSADI

**KUAMINIKWA  
 UWAJIBIKAJI  
 UAMINIFU  
 KUJITOlea  
 USHIRIKISHWAJI  
 AJIRA**

**KIKAO CHA BARAZA CHA JAMII YA MZIMA**

## WIKI 3

# CHANGAMOTO ZA GHARAMA YA JUU YA MAISHA

### TAZAMA: SIMULIZI

**W**atu wa jamii ya Mzima waliishi kwa amani na kufanya bidii maishani. Mazingira ya eneo hilo yaliwafaa wakulima, wafanya biashara, wavuvi na wafugaji. Wote waliweza kutosheleza mahitaji muhimu. Wazee na viongozi wa kidini waliaminika wakishughulikia masuala yote ya jamii, wakashauriwa kila mara kuhusu aina ya viongozi waliofaa kuchaguliwa. Viongozi wa kuchaguliwa waliwashauri pia.

Baada ya muda, viongozi waliochaguliwa walianza kuwavuruga baadhi ya wazee na viongozi wa kidini, jambo lililowafanya wengi wao kutoaminika tena. Waliwasahau wapigaji kura, wakajihusisha na visa vya ufisadi na hivyo kuathiri uchumi. Idadi ya wasio na kazi iliongezeka na gharama ya bidhaa muhimu kama vile unga, sukari, mafuta ya kupikia, petroli, stima na karo za shule ikapanda. Maisha yakawa magumu na familia zikatatizika kujikimu.

Mashirika ya utetezi wa haki za kiraia, wazee na viongozi wa kidini walioaminika waliobaki walikutana kujadiliana masuala yaliyokumba jamii ya Mzima. Walikubaliana kurejesha mfumo wa kushauriana, uadilifu na kuchagua tu viongozi waliochujwa na jamii. Katika uchaguzi uliofuatia, jamii ilichagua viongozi waliostahili, waadilifu na walioaminika. Bei za bidhaa muhimu zilishuka, watu wakapata mafanikio na utulivu wa akili.

### AMUA: UTATHMINI WA HALI HALISI

Kwa mujibu wa Shirika la Kitaifa la Takwimu la Kenya (KNBS), gharama ya sasa ya maisha ndiyo ya juu zaidi tangu 2017. Hali hiyo imezoroteshwa na mfumuko wa bei za kimataifa na madhara ya janga la COVID-19. Mambo yameharibiwa zaidi na usimamizi mbaya wa masuala ya fedha, kuimarishwa kwa ufisadi katika taratibu za bajeti, ukame wa kila mara, uhaba wa pesa za kugharamia matumizi ya serikali, ongezeko la kasi la madeni ya nchi, kuvunja sheria bila kujali kuadhibiwa, kiasi kikubwa cha mishahara ya watumishi wa umma, serikali kubwa kupindukia na matendo ya kifisadi miongoni mwa viongozi. Vita vya Ukraine vimeathiri mfumo dhaifu wa chakula ulimwenguni. Maeneo makubwa ya

ardhi za ufugaji na kilimo katika mashariki na kaskazini mwa Kenya yanakumbwa na hali mbaya ya hewa. Athari za mabadiliko ya hali ya anga zinaongezeka na kila mtu nchini anazihisi. Gharama ya juu na inayozidi kuongezeka ya maisha imezorotesha mambo na nchi inahitaji majadiliano ya kitaifa kuhusu jinsi ya kukabiliana na changamoto zinazotukumba. Ndiposa tunahitaji kuangazia hatua zinazoweza kutekelezwa za kujinasua kutoka katika hali ya sasa ya kiuchumi, na tuwe na mpango thabiti wa kuhakikisha pesa za umma hazipotei katika shughuli za kifisadi. Watu wakifahamu kuwa kodi zao hutumia kuzingatia uwazi na uwajibikaji, na wapate huduma wanazohitaji, watashirikiana na serikali.

Maaskofu Wakatoliki Kenya kwenye kikao chao maalumu cha Novemba, 2022, walisema: “Tunasikitishwa na gharama ya juu ya maisha nchini na mzigo mzito ambao watu wanabebeshwa. Bei za bidhaa muhimu za nyumbani kama vile unga, mafuta ya kupikia, gesi ya kupikia na stima, zimeongezeka kupita kiwango kinachoweza kufikiwa na Wakenya wa kawaida. Watu mamilioni wanahangaika katika juhudi za kutafuta chakula cha kila siku.”

Maaskofu wametoa miito ya hapo awali wakiomba walio katika mazingira magumu katika jamii wasaidiwe na kuhimiza waumini kujitokeza kuwasaidia ndugu na dada zao wahitaji.

Tukiwa nchi, tunahitaji kubuni mpango endelevu wa fedha kwa lengo la kuimarisha ustawi wa kiuchumi, kuinua uaminika wa hali ya kiuchumi, kukopa pesa tunazoweza kulipa kwa urahisi na kutoza kodi tukijali haki kwa wote. Sera imara za kiuchumi na utekelezaji kamili zitaaidia Kenya kukabiliana na changamoto za kiuchumi. Hujku taifa likiendelea kung’ang’ana kulipa madeni ya zaidi ya shilingi trilioni 10, tukumbuke kila mara tuishi kulingana na mapato yetu. Wakenya wote wanahofishwa na gharama ya madeni ya nchi na pana haja ya dharura ya kufanya mageuzi ya usimamizi ili kuimarisha uwazi kuhusu madeni ambayo nchi inadaiwa, na kuimarisha sera na miundo ya usimamizi wa madeni.

## **TAFAKARI YA KIROHO**

**Kutoka 20:1-17 au 20:1-3, 7-8, 12-17**

**1 Wakorintho 1:22-25**

**Yohane 2:13-25**

Amri Kumi ni kanuni za kutatanisha na zinazotupatia changamoto.

Mungu alitukabidhi amri hizo ili kuhakikisha tunaupata ulimwengu bora zaidi. Zinatupatia picha ya ulimwengu ambapo watu wanazingatia haki na ukarimu na ambapo kila mtu anaheshimiwa.

Kwa hakika, Yesu hawezi kuivumilia kamwe jamii ambapo hekalu ya Mungu, ambayo ni watu aliowaumba kwa mfano wake, inaishi maisha magumu na ya mateso yasiyovumilika yanayoendelezwa na wachache ambao haja yao kuu ni kuinua biashara zao. Kuimarisha haki, kuangamiza umaskini na kuujenga ufalme wa Mungu duniani ni jukumu la kila mmoja wetu na asasi za jamii.

Tukiwa Wakristo, ushirika wetu katika masuala ya kiuchumi unapaswa kuongozwa na kanuni zenye misingi na zilizotiwa nguvu na imani yetu. Tukiwa wafuasi wa Yesu na washiriki katika shughuli za kiuchumi za jamii yetu, tunahimizwa kujitahidi kuleta haki zaidi za kiuchumi tukizidi kukabiliana na gharama ya juu ya maisha. Uchumi unafaa kumnufaisha mtu wala sio mtu kunufaisha uchumi. Mwelekeo wa kiuchumi unaozingatiwa unapaswa kuiheshimu hadhi ya wanadamu wote itokayo kwa Mungu.

Ujumbe wa Kikristo unahusu msalaba ambao ni pingamizi kubwa kwa wote wanaotafuta ishara au busara. Lakini ni risala ya matumaini na wokovu kwa walioitwa na Mungu. Na ingawa mbinu za Mungu sio mbinu zetu, kwa kawaida yeye hufanya mambo kwa manufaa ya wote kwa nia tusizozielewa. Tunaweza kuamini kwamba njia zake zote ni njema na za busara.

Haki tuliyopewa na Mungu ya uhai na hakikisho la mambo muhimu maishani kama vile chakula, mavazi, makao, huduma za afya, elimu, mazingira salama na kujitosheleza kiuchumi zinapaswa kuheshimiwa na kudumishwa. Gharama ya maisha haifai kuwalazimisha watu kuchagua kati ya yaliyo muhimu maishani yafaayo kushughulikiwa na yepi ya kupuuziliwa mbali. Jamii, ikiwa ni pamoja na hatua za Serikali panapo uwezekano, ina jukumu la kuhakikisha nafasi za kujiendeleza kiuchumi zinapatikana, kutosheleza mahitaji muhimu na kuzingatia haki katika shughuli za kiuchumi.

Kuongezeka kwa gharama ya maisha husababisha ubaguzi wa kiuchumi. Tukiwa Wakristo, tunahitaji kufanya kila tuwezalo kuhakikisha hakuna yeyote anayebaguliwa wala kutengwa kiuchumi na kijamii. Tukiwa Kanisa, tunapaswa kujitahidi kuzuia hali hiyo kutokea. Tuwe watetezi wa watu wanaotatizika kujitetea na kuhakikisha sauti yao inasikika.



## **TENDA: MASWALI YA KUWAZIA**







- » Je, gharama ya juu ya maisha ina athari gani katika kaunti yako, jimbo, parokia au kijiji?
- » Je, ni hatua gani zinaweza kusaidia kukabiliana na hali mbaya ya kiuchumi nchini?
- » Je, unawezaje kukabiliana na changamoto za kiuchumi, kushuka kwa thamani ya shilingi na gharama ya juu ya maisha kwa familia zetu, vijiji, kaunti na nchi kwa jumla?

## **KUJICHUNGUZA**

- » Je, nimefanya juhudi kuelewa chanzo cha gharama ya juu ya maisha na kuchukua hatua za kibinafsi kukabiliana kikamilifu na hali hiyo?
- » Je, ni hatua gani ninazoweza kuchukua kupunguza gharama ya juu ya maisha?
- » Je, nimetoa mchango gani kwa hali ya sasa ya kiuchumi ya familia yangu?

## **MATENDO YALIYOPENDEKEZWA**

- » Jitolee kupunguza matumizi yasiyo muhimu.
- » Fanya mabadiliko katika bajeti, huku ukishirikisha watu wa familia, mashirika na sekta zote.
- » Shiriki katika majukwaa ya raia kuhusu uandalizi wa bajeti na ujitolee kupigana na ufiadini.
- » Zingatia mbinu rahisi za maisha.



## WIKI 4 IMANI KALI ZA KIDINI

### TAZAMA: SIMULIZI

**M**sito amehitimu kwa shahada ya digrii kutoka Chuo Kikuu cha Ukumbini. Ni Mkristo imara na majuzi alimaliza mafunzo yake ya Huduma ya Vijana kwa Taifa. Ni mchuuzi mwenye matumaini makubwa kwamba siku moja atafungua duka kubwa aina ya *supermarket* mjini Ukumbini.

Kwa bahati mbaya, alipatwa na ajali kwenye barabara kuu anapofanyia biashara baada ya lori kupoteza mwelekeo, likatoka nje ya barabara na kugonga watu waliokuwa wakitembea na pia baadhi ya wachuuzi kando ya barabara. Kufuatia ajali hiyo, serikali ya kaunti ilipiga marufuku uchuuzi kando ya barabara hiyo kuu. Alipotoka hospitalini, Msito alikuta amefungiwa nyumba kwa kukosa kulipa kodi kwa miezi kadha. Ombi lake la mkopo kutoka kwa kundi la vijana kanisani ambapo alikuwa na akaunti lilikataliwa. Uamuzi huo ulimvunja moyo na akaliasi kanisa.

Rafiki yake Potosha alikuwa na duka kubwa la jumla. Alimkaribisha na kumpatia riziki ya kila siku. Hatimaye, Msito aligundua kuwa Potosha alishiriki katika kundi la siri lililohubiri kuhusu maendeleo ya kibinafsi na kuunga mkono ulimbikazaji wa mali bila kujali mbinu ulizotumia kuipata. Kadhalika, lilitetea imani kali kama vile kuwa tayari kujitoa mhangana kwa sababu ya dini. Msito alitamani kuishi kama Potosha na akakubali washirikiane kibiashara kwa sharti Msito angeweke siri yote aliyoyashuhudia. Aliagizwa kuwa akikusanya vifurushi vilivyoletwa kila baada ya majuma mawili na watu asiowajua. Baadaye, aliingizwa kwa ibada za kutisha za usiku na utoaji kafara. Visa vingi vya watu walioshikwa mateka na hatimaye kupatikana maiti bila baadhi ya viungo vya mwili viliripotiwa. Jamii ilitiwa wasiwasi na mauaji hayo na kujitolea kushirikiana na polisi kushika doria mjini. Ugunduzi kwamba wote waliohusika na maovu hayo walikuwa washirika wa Potosha ambaye alishatoroka uliwashangaza wengi. Uchunguzi ulifichua kuwa alihusika na ulanguzi wa viungo vya miili ya watu akishirikiana na watu walioshukiwa uabudu wa shetani. Msito na wenzake walifungwa gereza kwa ujinga wao na tamaa ya utajiri wa haraka. Mipango ilianzishwa ya kufundisha na kushauri jamii ili kuinua uwezo wao wa kutambua wakipotoshwa kwa imani kali za kidini.

## AMUA: UTATHMINI WA HALI HALISI

Kuna tofauti ndogo sana kati ya imani kali za kidini na ugaidi. Wanaoendeleza maovu hayo hukatalia dhana kwamba ni baraka kuzusha vurugu na hata kusababisha maafa katika kumhudumia Mungu. Hata hivyo, dini zimetokeleza jukumu muhimu la kutoa mafundisho ya kiroho na maadili yanayozidi kuongoza watu ulimwenguni huu uliojaa taabu. Shabaha kuu ya dini ni kusaidia watu wasiangazie tu mali lakini waakisi pia haki, mapatano, upendo na kujitolea kwa manufaa ya wanadamu wote na jamii.

Kuna sababu mbali mbali za imani kali za kidini na zenye madhara makubwa kwa jamii kuenea. Baadhi madhehebu yameibua vurugu za kikabila zisizo na maana, kiasi cha baadhi ya watu kupoteza maisha kutokana na 'ufunuo mtakatifu' kutoka kwa miungu wanaoabudiwa na madhehebu hayo. Watu wanaojitenga na ada kama hizo huadhibiwa na kufukuzwa kutoka kwa familia zao.

Imani kali za kidini hualika ujinga na utumiaji mbaya wa maelezo ya kihistoria na hivyo kusababisha mizozano na uadui miongoni mwa wafuasi. Ufahamu mdogo wa habari kamili na mawazo kuhusu mafundisho ya dini ndio chanzo cha ushindani wa kidini. Matokeo ni wafuasi kama hao kupotoshwa na mashirika yao ya kidini, wanawachukia wengine na kushikilia misimamo mikali katika mahusiano na matendo yao.

Baba Mtakatifu Francis akihutubia kongamano ya la saba la viongozi wa dini za kimataifa na kitamaduni nchini Kazakhstan mnamo Septemba, 2022, alisema imani ya kweli ya dini inahitajika kukabiliana na imani kali za dini na kuuonyesha ulimwengu kuwa hatufai kutoamianiana au kuikashifu dini kana kwamba imekuwa chombo cha kuivuruga jamii ya kisasa. Dini si tatizo lakini ni sehemu ya kuleta ufumbuzi katika kujenga jamii yenye usawa zaidi."

Walanguzi wa binadamu na wanaohusika na shughuli haramu ya kung'oa viungo vya miili ya watu mara nyingi hujificha katika dini ili kuwanyemelea kwa urahisi wanaowalenga. Kuna viongozi wengi bandia wa kidini walioibuka na kujidai kusaidia wanaohitaji kulipiwa ada za matibabu hospitalini na mahitaji mengine. Wengine hujitajirisha kupitia kwa ibada za kidini.

Maaskofu Wakatoliki Kenya katika taarifa yao iliyolaani maafa ya Shakahola na kuhimiza kutekelezwa kwa sheria zinazosimamia mashirika ya kidini, walisema: "Inasikitisha sana tunaposhuhudia ukweli wa kuhofisha nchini ambapo watu wanaojidai kuwa manabii na viongozi wa vikundi vya kidini wameimudu sana ya

kuwatapeli Wakenya ambao ni wepesi wa kudanganywa kwa jina la dini. Kwenye harakati hizo, wafuasi wasio na makosa wamepoteza pesa, mali na sasa maisha. Tunawaarifu Wakenya kwamba imani kali za dini ni hatari na lazima wawe macho kila mara. Viongozi wa vikundi hivyo vya kidini vyenye imani kali huwateka akili wafuasi wao na kuwafanya kuamini kwamba wao (viongozi) hawawezi kufanya makosa na ni wao pekee wanaoufahamu ukweli.”

Dini zote zinafaa kuhubiri umuhimu wa kuvumiliana ili kuimarisha hali ya watu kuishi pamoja kwa amani na umoja katika jamii. Serikali ichukue hatua kali na kuonyesha ina nia njema ya kulinda watu kutokana na mbwa mwitu. Isihofie kukataa kusajili vituo vya kuabudia ambavyo havijatimiza kanuni hitajika. Uchunguzi wa dharura wa mfumo uliopo ufanywe ili kutambua viongozi wa kidini wanaotafuta kuabudiwa na wafuasi, na pia asasi zinazotoa mafunzo yasiyofaa. 1 Yohane 5: 20-21 yasema: “Nasi pia twajua ya kwamba Mwana wa Mungu amekuja, naye ametupa sisi ufahamu ili tupate kumjua yeye aliye Kweli. Nasi tumo ndani yake yeye aliye Kweli, yaani, ndani ya Yesu Kristo Mwanawe. Yeye ndiye Mungu wa kweli na uzima wa milele. Watoto wapendwa, jilindeni nafsi zenu kutokana na sanamu. Amen.”

## **TAFAKARI YA KIROHO**

**2 Mambo ya Nyakati 36:14-16, 19-23**

**Waefeso 2:4-10**

**Yohane 3:14-21**

Somo la kwanza linatukumbusha kuwa kuwachagua miungu wengine au kuabudu kwa njia isiyofaa, sawa tu na dhambi yoyote, kuna adhabu yake. Tunapomkaidi Mungu, huwa tunajitoa kwake atuhukumu. Hata hivyo, Mungu bado ni mwenye huruma na huwa tayari kutusamehe na kuturejeshea upendo wake.

